# MwanaHisa

CRDB BANK PLC

Toleo La Septemba, 2018



## Yaliyomo

2 Maazimio ya Mkutano Mkuu wa 23

4 Utekelezaji wa Mkakati Mpya wa Biashara (2018 - 2022) waanza

5 Je wajua? Fedha za kidijitali hung'ata na kupuliza!

6 Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Benki ya CRDB katika picha

7 Benki ya CRDB yang'ara Kimataifa

8 Kibonzo

@crdbbank

@CRDBBankPlc

crdbbankplc

CRDB Bank Plc

## ANUANI

Mhariri Mwanahisa

CRDB Bank Plc
Office Accommodation Scheme
Mtaa wa Azikiwe, Ghorofa ya 4
S. L. P. 268, Dar-es-Salaam
Simu Na. 022 - 2114237, 022-21174421 - 7
Fax na. 022 - 2131005
investorrelations@crdbbank.com au
shareholders@crdbbank.com
www.crdbbank.com

CRDB BANK
The bank that listens

# MAAZIMIO YA MKU




*Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei akiwasilisha Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 31, Disemba 2017.*


**Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ulifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC), Ukumbi wa Simba jijini Arusha tarehe 19 Mei, 2018 ambapo masuala mbalimbali yalijadiliwa na maazimio kadhaa kufanyika. Mkutano Mkuu wa Wanahisa hufanyika kila mwaka kwa mujibu wa Katiba ya Benki, matakwa na taratibu za Utawala Bora. Kama ilivyo desturi, Mkutano Mkuu ulitanguliwa na Semina ya Wanahisa iliyofanyika tarehe 18 Mei 2018 katika ukumbi wa Simba na kufuatiwa na hafla fupi iliyofanyika Hoteli ya Mount Meru.**

# TANO MKUU WA 23

Hafla hiyo ilitoa nafasi adhimu kwa wanahisa kujadiliana, kubadilishana mawazo na kufahamiana miongoni mwao na wakurugenzi na menejimenti nzima ya Benki hivyo kuimarisha mahusiano kati ya wanahisa na benki yao.

Wanahisa waliohudhuria semina walipata elimu na maarifa kuhusu uwekezaji, umuhimu wa kuandika wosia, na kufahamu matumizi ya fedha za kidijitali na namna mifumo yake inavyofanya kazi na athari zake kiusalama.

Mkutano Mkuu ulihudhuriwa na wanahisa takriban 900 kutoka mikoa na maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Asilimia 79 ya hisa za Benki ziliwakilishwa. Wanahisa walishiriki kikamilifu na kutoa maoni na kuuliza maswali ambayo yatasaidia Bodi na Menejimenti kuboresha uendeshaji.



*Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB Bw. Abeid Mwasajone akiongoza Mkutano huo.*

**Yafuatayo ni Maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB :**

- ✓ Gawio la shilingi 5 kwa kila hisa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Disemba 2017.
- ✓ Ada ya Wakurugenzi ya shilingi 818,478,576/= kwa mwaka 2018 .
- ✓ Bw. Apollo Temu na Dkt. Faustine Karrani Bee walichaguliwa kuwa wakurugenzi wapya wa Bodi kutoka Kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja .
- ✓ Bi. Rose Felix Metta alichaguliwa kwa mara nyingine kuwa mjumbe wa Bodi kutoka kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi.
- ✓ Kampuni ya Ernst & Young Tanzania iliidhinishwa kuwa Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki ya CRDB kwa mwaka 2018.
- ✓ Bodi ya Wakurugenzi ifikirie upya uamuzi wa kustaafu wa Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Charles S. Kimei kutokana na changamoto za kibiashara zinazoikabili Benki na sekta ya kifedha kwa sasa.
- ✓ Mkutano Mkuu wa 24 wa Wanahisa ufanyike jijini Arusha tarehe 18 Mei, 2019 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) kwenye Ukumbi wa Simba.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB Bw. Ally Hussein Laay akiwasilisha taarifa na matokeo ya kifedha kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2017 wakati wa Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 19, Mei 2018 Jijini Arusha .*

# Utekelezaji wa Mkakati Mpya wa Biashara (2018 - 2022) waanza

**Benki ya CRDB imeanza utekelezaji wa mkakati Mpya wa Biashara wa Miaka Mitano (2018-2022) unaolenga kuleta mageuzi ya utendaji kuanzia ngazi ya tawi, kuboresha ufanisi na tija na kuimarisha mchakato wa kusimamia vihatarishi vya mikopo na kutumia mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma kwa wateja. Maudhui ya mkakati mpya wa biashara ni; 'Safari ya Mageuzi ya Kidijitali.' Mkakati huo umepitishwa na bodi ya wakurugenzi baada ya tathmini ya utekelezaji wa mkakati uliopita (2013-2017) kufanyika.**

Mkakati uliopita ulipata mafanikio kadhaa ikiwemo kupanuka kwa mtandao wa vituo vya huduma,ambapo jumla ya vituo vidogo vya huduma na matawi ya kawaida yaliongezeka kutoka 93 mwaka 2012 hadi matawi 260, mashine za kuweka na kutoa fedha (ATMs) kuongezeka kutoka 245 hadi 550 pamoja na uanzishwaji wa huduma za benki kwa njia ya mtandao wa simu ya mkononi (Simbanking na Simaccount) huduma za benki kwa mtandao wa intaneti,pamoja na kuanzishwa kwa mfumo wa kutolea huduma za Benki ya CRDB kupitia kwa mawakala wa Fahari Huduma.

Mkakati mpya umejengwa katika nguzo kuu tatu. Nguzo ya kwanza ni kuongeza ufanisi na tija, ambayo inajumuisha mageuzi ya utendaji wa matawi na taratibu za ukusanyaji amana na utoaji wa mikopo. Moja ya vipimo muhimu vya utendaji itakuwa uwiano kati ya gharama na mapato. Azma hii itatekelezwa kwa kuboresha mifumo na taratibu za utendaji ili kuwawezesha wafanyakazi walio wengi zaidi kujihusisha moja kwa moja na shughuli za mauzo na kuhudumia wateja.

Nguzo ya pili ni kujenga Benki ya kisasa ambayo michakato yake inaendeshwa kidijitali na kuwezesha wateja kupata huduma bora katika maeneo yote kama vile mashine za kutoa na kuweka fedha (ATMs), vituo vya mauzo (PoS), intaneti *banking, Simbanking* na mawakala wa FahariHuduma. Awamu ya kwanza ya safari ya mageuzi ya kidijitali imekamilika na utekelezaji wa awamu ya pili unaendelea. Mageuzi ya kidijitali yataimarisha uwezo wa Benki na kampuni zake tanzu kutoa bidhaa na huduma bora, kuongeza ufanisi na kuridhisha wateja. Nguzo ya tatu ni kuwekeza katika vitendea kazi na mifumo yetu ya kielektroniki ili kuhakikisha Benki inaendelea kutoa huduma bora wakati wote. Hatua hii inajumuisha kuimarisha ufanisi wa mfumo mkuu wa Benki na mifumo mingine ya utendaji na usimamizi.


CRDB BANK
The bank that listens

# Je wajua? Fedha za kidijitali hung’ata na kupuliza!

**Fedha za kidijitali (crypto currencies) zimekuwa gumzo nchini Tanzania na duniani miaka ya hivi karibuni, watu wengi wakitamani kulamba asali hiyo, huku wengine wakihofia madhara yake. Sambamba na shauku hiyo mamlaka za uthibiti ndani na nje ya nchi zimekuwa na mitazamo tofauti kuhusu fedha za kidigitali. Hivi karibuni Benki Kuu imetoa tahadhari kutokana na uwezekano wa watumiaji wa fedha hizo kupata hasara kwa kuwa fedha hizo hazina mfumo wa udhibiti hapa nchini na kimataifa. Kwa tafsiri ya haraka fedha za kidigitali zinaonekana kama asali inayovutia watu wengi kuilamba na wakati huo huo zinakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoleta uchungu ndani yake.**

**Fedha za kidijitali ni nini?**

Fedha za kidijitali ni mfumo wa *kielektronik*i wa malipo taslimu. Fedha hizo zimetengenezwa na kuhifadhiwa *kidijitali* katika mfumo maalum unaoitwa *blockchain* kwa kutumia lugha mficho (*encryption*). Kuna aina nyingi za fedha au sarafu za kidijitali, lakini Bitcoin ndio maarufu zaidi ulimwenguni. Sarafu hiyo inaundwa na kutumika kielektroniki na inaweza kutumika kufanya manunuzi kielektroniki na haina tofauti na matumizi ya kawaida ya dola/shilingi na inahamishika kati ya mtu mmoja na mwingine. Kumbukumbu za malipo za Bitcoin zinahifadhiwa katika mfumo unaoitwa *Blockchain* kwa kutumia kiwango chake cha akaunti (Bitcoin). Katika matumizi ya Bitcoin hakuna ada ya miamala ya ndani ya nchi na kimataifa.

Inaaminika kuwa mvumbuzi wa Bitcoin ni raia wa Japan Bw. Satoshi Nakamoto, mnamo mwaka 2009. Alianzisha sarafu hiyo kwa lengo la kurahisha miamala na kuondoa urasimu wa mifumo ya usimamizi. Baadhi ya faida za fedha za kidijitali ni kutokuwepo kwa urasimu kwa kuwa hakuna mamlaka ya usimamizi katika matumizi yake na kuna usiri katika miamala inayofanyika. Mtu yeyote anaweza kujiunga na hakuna mamlaka inayojihusisha na kushusha au kuongeza thamani ya fedha ya Bitcoin

Kutokana na umaarufu wake kuongezeka na baadhi ya watu nchini Tanzania kuanza kutumia mfumo huo, tahadhari imetolewa na



*Mkurugenzi wa Hazina na Soko la Mitaji wa Benki ya CRDB Bw. Alex Ngusaru akiwasilisha mada kuhusu fedha za ‘kidijitali’ wakati wa semina ya wanahisa wa Benki hiyo iliyofanyika siku moja kabla ya Mkutano Mkuu wa 23 wa Wanahisa.*

Benki Kuu kuwa watumiaji wanaweza kupata hasara kwa kuwa mfumo huo haujatambulika rasmi nchini na hakuna udhibiti wake.

Watumiaji wa fedha za kidijitali za Bitcoin wanaweza kupata hasara kwa kuwa miamala yote inafanyika kidijitali na mfumo huo unapatikana *kielektroniki* tu na hauna mmiliki wala ofisi inayotambulika duniani inayosimamia matumizi yake na miamala ikishafanyika haiwezi kurejeshwa. Hatari nyingine ni kuwa thamani ya fedha hizo hubadilika kila mara na matatizo ya kiufundi yanaweza kutokea na kumletea hasara mtumiaji.

# Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Benki ya CRDB katika picha



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Dkt. Charles Kimei akibadilishana mawazo na baadhi ya wanahisa wa Benki hiyo wakati wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa uliofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa-AICC, Jijini Arusha.



Mwanahisa akisoma kitabu cha Mkutano Mkuu.



Mwanahisa akichangia maoni.



Balozi wa Denmark nchini Tanzania Mh. Einar Jensen akifuatilia Mkutano Mkuu wa Wanahisa.






Wagombea kutoka kundi la Wanahisa wenye Hisa chini ya asilimia moja, Bw. Apollo Temu (kushoto) na Bw. Faustine Karrani Bee wakitoa neno la shukrani baada ya kuchaguliwa kuwa wajumbe wa Bodi.

# Benki ya CRDB yang'ara Kimataifa

***Benki ya CRDB imeendelea kung'ara kitaifa na kimataifa kwa kutunukiwa tuzo mbalimbali kutokana na ubora wa huduma na bidhaa zake.***

Mwezi Mei mwaka 2018, Benki ya CRDB ilitangazwa kuwa benki bora ukanda wa Afrika Mashariki wakati wa hafla maalum ya utoaji tuzo kwa benki bora barani Afrika iliyofanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo Afrika-AfDB nchini Korea Kusini.

Tuzo hiyo ni muendelezo wa mafanikio ya Benki ya CRDB kutokana na kuwekeza katika kuboresha huduma na bidhaa zake kwa wateja na kujikita kwenye mageuzi ya kidijitali yanayolenga kutoa huduma kwa kutumia njia mbadala kama vile *Simbanking, Simaccount, intaneti banking* na mawakala wa FahariHuduma.


Benki ilitwaa tuzo mbalimbali mwaka 2017 zikiwemo: Benki Bora nchini kwa kuwezesha biashara; Cheti cha kutambua mchango wa Benki kifedha; *Benki inayoongoza kwa kuwajibika kijamii nchini; Benki bora ya wateja wadogo na wa kati; Benki bora kwa kuwasilisha taarifa za fedha na Benki bora kwa ubunifu Afrika Mashariki.*



*Ujumbe wa Benki ya CRDB ukiongozwa na mjumbe wa Bodi Prof. Mohamed Warsame katika picha ya pamoja baada ya kupokea tuzo ya Benki Bora Kanda ya Afrika Mashariki iliyotunukiwa Benki ya CRDB wakati wa hafla maalum nchini Korea Kusini hivi karibuni. Wengine katika picha ni; Mkurugenzi wa Fedha Bw. Frederick Nshekanabo (wa kwanza kushoto), Mkurugenzi wa Hazina na Soko la Mitaji Bw. Alex Ngusaru, Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa Bw. Goodluck Nkini (wa kwanza kulia) na Meneja wa Rasilimali na Madeni Bw. Joseph Maji.*

# MAMA FAIDA NA BABA MTAJI

## WAKIELEZEA UMUHIMU WA WANAHISA KUCHUKUA GAWIO






CRDB BANK
The bank that listens